

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**  
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**05**

**SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Time: 2:30 Hours.**

**MAJIBU**

**Mwaka: 2021**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali matano (5)
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama thelathini (30) na sehemu B ina alama ishirini (20).

maktaba.tetea.org



SEHEMU A (Alama 30)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku.

(i) Nini kazi ya antenna katika redio?

- A. Kurekebisha sauti
- B. Kuchukua mawimbi angani
- C. Kurekebisha stesheni
- D. Kupaza sauti

**B. Kuchukua mawimbi angani**

Antenna hufanya kazi ya kupokea mawimbi ya redio kutoka angani ili yaweze kuchakatwa na kutoa sauti.

(ii) Ni vifaa vipi vya kisasa hutumika katika mawasiliano?

- A. Simu, redio na runinga
- B. Ngoma, filimbi na runinga
- C. Redio, gazeti na baragumu
- D. Simu, ngoma na baragumu

**A. Simu, redio na runinga**

Vifaa hivi hutumia teknolojia ya kisasa katika kuwasilisha taarifa na ujumbe.

(iii) Ni kwa namna gani mawasiliano ya picha na maandishi huoneshwa katika runinga?

- A. Kupitia spika
- B. Kupitia skrini
- C. Kupitia antena
- D. Kupitia rimoti

**B. Kupitia skrini**

Skrini ndiyo sehemu ya runinga inayobeba picha na maandishi yanayoonekana.

(iv) Ni kampuni ipi haitoi huduma za mitandao ya simu Tanzania?

- A. TTCL
- B. VODACOM
- C. TECNO
- D. TIGO

### C. TECNO

TECNO ni kampuni ya kutengeneza simu, siyo mtoa huduma za mitandao ya simu.

(v) Simu zinazopigwa unapohitajika msaada wa haraka zinaitwaje?

- A. Simu za upepo
- B. Simu muhimu
- C. Simu za sauti
- D. Simu za dharura

#### D. Simu za dharura

Simu hizi hutumika kupata msaada wa haraka wakati wa hatari.

2. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuoanisha dalili za magonjwa katika Orodha A na magonjwa husika katika Orodha B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

<b>Kundi A</b>	<b>Majibu</b>	<b>Kundi B</b>
(i) Kukakamaa viungo na kupinda shingo	<b>(C)</b>	C. Pepopunda
(ii) Kuota vipele vidogo vidogo mwilini	<b>(E)</b>	E. Surua
(iii) Kujisaidia kinyesi kama maji yaliyoshewa mchele	<b>(G)</b>	G. Kipindupindu
(iv) Kukojoa mara kwa mara	<b>(B)</b>	B. Kisukari
(v) Kutoa sauti kama filimbi wakati wa kupumua	<b>(F)</b>	F. Pumua

3. Jibu vipengele (a) hadi (e) kwa kuandika hatua za uchunguzi wa kisayansi zilizo katika kisanduku. Hatua zilizopo: Kuchambua data, Kutafsiri matokeo, Kubuni dhanio, Kufanya jaribio, Kubainisha tatizo.

(a) Hatua ya kwanza

#### Kubainisha tatizo

(b) Hatua ya pili

**Kubuni dhanio**

(c) Hatua ya tatu

**Kufanya jaribio**

(d) Hatua ya nne

**Kuchambua data**

(e) Hatua ya tano

**Kutafsiri matokeo**

### SEHEMU B (Alama 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

4. Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu vipengele (a) hadi (e) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Uvaaji wa nguo chafu husababisha harufu mbaya mwilini na wakati mwingine magonjwa ya ngozi. Nguo safi humfanya mtu kuonekana nadhifu na wa kuvutia. Ili kufanya nguo ziwe safi, ni lazima zifuliwe kwa kutumia maji safi na sabuni. Baada ya nguo kukauka zinapaswa kupigwa pasi ili kuua vimelea vya magonjwa. Pia upigaji nguo pasi unamfanya mvaaji aonekane nadhifu. Nguo zikishakuwa safi zinaweza kuvaliwa au kuhifadhiwa sehemu safi na kavu, kama vile sandukuni au kabatini.

**Maswali:**

(a) Ni vifaa gani vinahitajika wakati wa ufuaji nguo?

(i) **Maji safi**

(ii) **Sabuni**

(b) Athari ya kuvaa nguo chafu ni nini?

Athari ni **kusababisha harufu mbaya mwilini na magonjwa ya ngozi.**

(c) Kwanini tunapiga nguo pasi? Toa sababu moja

Tunapiga nguo pasi **ili kuua vimelea vya magonjwa.**

(d) Nini kinaua vimelea wakati wa kupiga pasi?

**Joto la pasi** huua vimelea vya magonjwa.

(e) Kwa nini nguo safi huhifadhiwa kabatini au sandukuni?

Huhifadhiwa huko **ili ziendelee kuwa safi na kavu.**

5. Tumia vifaa vilivyooneshwa katika picha kujibu vipengele (a) hadi (e). Andika jibu katika nafasi uliyopewa.

(a) Kifaa kipi kinatoa kipimo kisicho rasmi?

**Ndoo**

(b) Kifaa kipi hupima ujazo wa maji kwa usahihi?

**Silinda ya kupimia**

(c) Urefu wa dawati hupimwa kwa kifaa kipi?

**Rula**

(d) Kifaa kipi hutumika kupima uzito wa kitu?

**Mzani**

(e) Kwa nini kipimo kilichopimwa na rula ni kipimo rasmi?

Kwa sababu **rula ina vipimo vilivyokubaliwa kitaifa na kimataifa.**